# MKURUGENZI BI. ZAHARA MSANGI AMSHUKURU MHE. RAIS KWA KAZI KUBWA ALIYOIFANYA KIPINDI CHA MIAKA 2 NA MIEZI 5 HALMASHAURI YA (W) YA MKINGA



**Na: Nassoro Rashid**
**MDC Habari**

Mara nyingi wenye hekima na busara husema, asiyeshukuru kwa kidogo hata kwa kikubwa hawezi kushukuru.

Aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga Bi. Zahara Abdul Msangi ambaye kwa sasa amehamishiwa Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga katika Mkoa wa Kilimanjaro kupitia taarifa ya uteuzi wa Disemba 12, 2023 amemshukuru Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kumuamini tena katika nafasi hiyo.

Akizungumza kwa nyakati tofauti na Watumishi, Wakuu wa Idara pamoja na Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango Mkurugenzi Bi. Zahara amesema katika miaka (2) na miezi mitano (5) aliyofanya kazi Halmashauri ya Mkinga ameweza kutekeleza maono mbalimbali ya Serikali ya awamu ya Sita kupitia idara na vitengo vyake mbalimbali.

*INAENDELEA UK. 2*

INATOKA UK. 1



*"Kwa niaba ya Wananchi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga, napenda kumshukuru sana Mhe. Rais Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa aliyoifanya katika kipindi cha miaka miwili na miezi mitano nikiwa Mkurugenzi Mtendaji katika Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga ". Alisema Bi. Zahara Msangi.*







Aidha Mkurugenzi huyo ameyataja mafanikio mbalimbali ambayo yamewezeshwa na Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kipindi cha miaka hiyo ikiwemo;

**KUPITIA MAPATO YA NDANI**, Mkurugenzi kwa kushirikiana na Kamati ya Wataalamu (CMT), Waheshimiwa Madiwani na Watumishi amefanikiwa kuongeza mapato ya ndani kutoka Shilingi 1,232,759,984.89 kwa mwaka wa fedha 2020/21 hadi Shilingi 2,605,967,000 mwaka 2022/23, ambapo katika kipindi chote hicho kwa nyakati tofauti mapato hayo ya ndani yaliweza kutekeleza miradi mbalimbali;

*" Ujenzi wa Zahanati kubwa ya kisasa katika Kata ya Mayomboni ambapo zahanati hii ina eneo la wagonjwa wa nje (OPD), jengo la Mama na Mtoto (RCH) na pia sehemu ya Wanawake kujifungulia (Maternity), Ujenzi wa Nyumba ya Walimu (Mbili kwa moja) Shule ya Msingi Ng'ombeeni katika kata ya Daluni. Ukarabati wa miundombinu jengo la Utawala la Halmashauri, Ujenzi wa jengo la Mama na Mtoto (RCH) katika Kata ya Sigaya Kijiji cha Kilulu Duga, Ujenzi wa Madarasa mawili na Ofisi ya Walimu katika Shule ya msingi Kinyatu kata ya Mkinga ". Alisisitiza Mkurugenzi Bi. Zahara.*

Sambamba na hayo umaliziaji wa vyumba 4 vya madarasa Shule ya Msingi Mbamba kofi na Matundu ya vyoo, Uboreshaji wa miundombinu ya stendi ya mabasi Manza ambapo choo cha kisasa kimejengwa, Vibanda vya maduka, Ofisi ya ukusanyaji ushuru na Ofisi ya Askari wa Jeshi la polisi pamoja na miundombinu ya maji na umeme katika eneo lote, pia Ukarabati wa Hosteli ya wasichana iliyoungua moto shule ya sekondari Lanzoni, Ukamilishaji wa Ujenzi wa Bweni Shule ya Sekondari Maramba.

Kadhalika uzalishaji wa miche ya mkonge katika tarafa ya Mkinga na Maramba na kuigawa bure kwa wakulima, Utoaji wa Mikopo kwa

INAENDELEA UK. 3

INATOKA UK. 2



makundi ya Wanawake, Vijana na Watu wenye ulemavu kwa kutumia 10% ya mapato ndani ya Halmashauri, Ujenzi wa Ofisi ya kata ya Mnyenzani, Ukamilishaji wa vyumba vya madarasa Shule ya Msingi Cheto, Ujenzi wa barabara inayoingia katika soko la samaki Kidoviani pamoja na Ujenzi wa Mageti na Vibanda vya kukusanyia mapato.

Katika hatua nyingine Mkurugenzi Bi. Zahara amesema kupitia Ruzuku kutoka Serikali Kuu na Wafadhili Halmashauri ilifanikiwa kutekeleza Miradi mbalimbali ikiwemo kwenye,

**SEKTA YA AFYA.** Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ambayo kwa sasa imeanza kutumika, Ujenzi wa kituo cha Afya Daluni, Ukamilishaji wa maboma ya Zahanati za Mavovo, Magaoni, Perani, Muzi Kafishe, Churwa, Kwekuyu, Mzingi Mwagogo, Hemsambia, Mwakikonge, Mwakikoya, Segoma na Matemboni ambapo kati ya Zahanati hizo nane zimesajiliwa na kuanza kutoa huduma kwa Wananchi.

*Jengo la Hospitali ya Wilaya*



Pia ujenzi wa Nyumba ya Watumishi wa Afya aina ya Tatu kwa moja (3x1) katika Kijiji cha Mazala Kilifi Zahanati ya Kilifi, Ujenzi wa Nyumba tatu za watumishi katika Zahanati za Muzi Kafishe, Zahanati ya Perani na Zahanati ya Kwekuyu, Ununuzi wa vifaa tiba kwa ajili ya Vituo vya Afya na Zahanati pamoja na Jokofu kwa ajili ya kuhifadhi Maiti katika kituo cha Afya Mkinga HC

**SEKTA YA ELIMU SEKONDARI:** Ujenzi wa Shule mbili mpya za Sekondari katika kata za Kigongoi Magharibi (Kwekuyu sekondari) na kata ya Parungu Kasera, Uanzishaji wa Shule Mpya ya Sekondari Doda, Ujenzi wa vyumba vya Madarasa 76 katika Shule za Sekondari, Ujenzi wa matundu ya vyoo 56 katika shule za Sekondari, Ujenzi wa Ofisi za Waalimu 24 katika shule za sekondari, Umaliziaji wa vyumba 8 vya Madarasa katika shule za sekondari, Utengenezaji wa Viti na Meza

Kadhalika ujenzi wa Mabweni mawili Shule ya Sekondari Zingibari, Umaliziaji wa Bweni la Wasichana Shule ya Sekondari Mkinga Leo, Umaliziaji wa Bwalo la Chakula Shule ya Sekondari Mkinga Leo pamoja na Upanuzi wa Shule ya Sekondari ya Mapatano ambapo kiasi cha Shilingi Bilioni 7 kitatumika katika mradi huo unaofadhiliwa na shirika la Mfuko wa Abbott.

INAENDELEA UK. 4





Shule ya Sekondari Parungu Kasera

**KUPITIA ELIMU MSINGI,** Halmashauri pia imefanikiwa utekelezaji wa Ujenzi wa Shule Mpya ya Awali na Msingi Maramba JKT iliyopo kata ya Maramba, Umaliziaji wa Bweni la Watoto wenye Mahitaji Maalum na uzio katika Shule ya Msingi Maramba JKT, Ukarabati wa Kituo cha Walimu cha kujifunzia (TRC) Shule ya msingi uhuru, Ujenzi wa vyumba vya madarasa 46 katika shule za Msingi.

*“ Sambamba na hayo Ujenzi wa ofisi za waalimu 23 katika shule za msingi, Umaliziaji wa vyumba vya Madarasa 24,Ujenzi wa nyumba ya Walimu (2 kwa 1) katika kata za Mayomboni, Boma na Mnyenzani, Ujenzi wa matundu ya vyoo 116 katika shule za Msingi pamoja na jumla wa madawati 810 yametengenezwa shule mbalimbali za msingi ”. Aliongezea Bi. Zahara*













1. Shule ya Msingi Maramba JKT 2. S/Msingi Mtimbwani
3. Nyumba ya Mwalimu (2x1 ) Jasini 3. N/Mwalimu Mkambani

INAENDELEA UK. 5

INATOKA UK. 4



KITUO CHA WALIMU


ZAHANATI YA BANTU

Katika hatua nyingine Mkurugenzi Bi. Zahara amesema katika kipindi chote hicho Sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi pia imepiga hatua ambapo kupitia **SEKTA YA KILIMO** Halmashauri imefanikiwa kuanzisha Vitalu vya uzalishaji wa miche ya Mkonge katika Tarafa ya Mkinga na Maramba na kugawa mbegu bure kwa Wananchi, Shamba la Miche ya Korosho katika Kijiji cha Mwakikonge Kata ya Duga, Pembejeo za Kilimo na Mbolea ya Ruzuku Tani 51 zilisambazwa kwa wakulima na jumla ya lita 5168 za dawa ya kupulizia korosho zilisambazwa kwa Wakulima pamoja na Vitalu vya Miche ya Korosho katika Vijiji vya Horohoro Boda na Horohoro Kijijini.

*"Pia kupitia SEKTA YA MIFUGO, Halmashauri kwa kushirikiana na Wizara husika tumefanikiwa kujenga Mnada wa Mifugo wa Horohoro Mpakani ambao ni wa kisasa, Uanzishwaji wa Minada ya Msingi miwili katika eneo la Mwakijembe, Sokonoi na Ng'ombeni, Ujenzi wa Majosho ya kuogeshea mifugo katika Kijiji cha Kibewani kata ya Sigaya na Mkota kata ya Mwakijembe pamoja na kuanzisha Mradi wa Vijana wa Banda la kuku." Alisisitiza Mkurugenzi Bi. Zahara.*




Mnada wa Mifugo wa Mpakani - Horohoro

Kadhalika kupitia **SEKTA YA UVUVI** Halmashauri imefanikiwa katika utekelezaji wa ujenzi wa jengo la Ofisi za BMU pamoja na ujenzi wa Soko la kisasa zote katika kata ya Moa ambapo ujenzi wa Soko bado unaendelea.

Kwa namna nyingine Bi.Zahara amesema kupitia **SEKTA YA MALIASILI NA UHIFADHI WA MAZINGIRA** Halmashauri imefanikiwa kupanda miti 856,701 kwa mwaka wa fedha 2021/22 sawa na 57.1%, na mwaka 2022/23 miti 1,056,000 sawa na 70.4% ya lengo la kupanda

INAENDELEA UK. 6

INATOKA UK. 5


miti 1,500,000 kila mwaka, uhuishwaji wa Kamati 20 za Usimamizi wa Maliasili katika vijiji 20, upimaji wa Misitu sita ya vijiji katika zoezi la Maandalizi ya Matumizi Bora ya Ardhi yaliyofanyika katika vijiji 9.



Sambamba na hayo jumla ya Mabwawa 6 na chanzo cha maji cha mto Muzi viliwekewa Mawe ya vigingi kwa ajili ya ulinzi wa vyanzo hivyo, Vijana 6 kutoka katika vijiji vinne wamepelekwa chuo cha Litui Mkoa wa Ruvuma kupata mafunzo ya Skauti wa Wanyamapori wa Vijiji pamoja na kutoa mafunzo kwa Vikundi vya usasi kutoka katika vijiji nane vyenye changamoto ya Wanyamapori hatari na kugawa Vifaa vya kukabiliana na Wanyamapori hatari kwa kushirikiana na Mamlaka ya Wanyamapori Tanzania (TAWA) pamoja na TANAPA.

Kwa namna nyingine Bi. Zahara amesema kupitia Idara ya **UTAWALA,** Halmashauri imefanikiwa kujenga Nyumba ya Mkurugenzi, ununuzi wa Magari matatu kwa ajili ya usimamizi na ufuatiliaji wa shughuli za Halmashauri, malipo ya malimbikizo ya mishahara na madeni ya Watumishi kadhalika jumla ya Watumishi 402 wameajiriwa katika sekta mbalimbali ambapo katika Sekta ya Afya Watumishi 85, na sekta ya Elimu Msingi na Sekondari Watumishi 87 mpaka kufikia sasa.




Ama kwa hakika kipindi chote alichokuwa akifanya kazi Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga, kwa kushirikiana na Waheshimiwa Madiwani, Kamati ya Wataalamu pamoja na Watumishi kimekuwa ni kipindi chenye mafanikio mengi ambapo kwa ujumla Mkurugenzi Bi. Zahara ana kila sababu ya kuendelea kumshukuru Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuiwezesha Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga kwa namna moja ama nyingine kuhakikisha maono, dhamira na malengo makubwa ya Serikali ya Awamu ya Sita yanafikiwa ili kusudio la utoaji wa huduma bora kwa wakati iwafikie Wananchi wote kwa kiwango kilekile, ameongezea kusema kuwa anaahidi kuendelea kutekeleza majukumu yake ipasavyo katika Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga ili kutimiza dhamira ya Mhe. Rais ya kuwapatia huduma bora Wananchi waishio Mjini na Vijijini.

Kazi Iendelee.